


Kitabu hiki ni mali ya...



Baylor College of Medicine and Texas Children's Hospital, both located in Houston, Texas, operate a network of clinical centers that focus on child and family-centered healthcare and education in 6 countries in Africa as well as Romania.



“Agness, Jonathan
–zimeni TV. Ni
muda wa kulala.”

“Lakini mama,
tunaweza kuendelea
kuangalia kidogo?”
alisema Jonathan,
akionyesha wasiwasi
kidogo.

Mama akatabasam.
“Kijana wangu,”
alisema “unajua saizi
ni saa mbili usiku
ni muda wa kulala.
Mnatakiwa mlale ili
kesho mujiandae kwa
kuwahi shule.”

“Saizi ni muda wa
kuswaki, kuosha uso
na kunywa dawa,”
alisema hayo kwa
kutabasam, “haya
twendeni.”





“Mama, naomba nikuulize swalii?” alisema Agness akipiga mswaki.

“Niulize mwanangu, ni kitu gani?” aliuliza mama Agness.

“Kila siku jioni kabla ya kwenda kulala, tunakunywa dawa. Ni kwanini tunatakiwa kufanya hivi?”

A close-up illustration of a woman's face. She has dark brown skin, large expressive eyes, and a wide, joyful smile showing her teeth. She is wearing a yellow shirt. Her right hand is visible, holding a white toothbrush with a blue cap and a tube of white toothpaste with a green label.


“Wanangu mnatakiwa kunywa dawa kila siku
kusaidia askari wetu.

Jonathan alichanganyikiwa kidogo, “askari wetu?
“Ni wakina nani hao?” Sijawahi kuwaona hao
askari.”




“Uko sahihi,
Jonathan,” alisema
mama yao.

“Huwezi kuwaona
hao askari kwa
sababu ni wadogo
wadogo sana.”



“Ndani ya miili
yetu kuna askari
wengi wadogo
wadogo. Haijalishi
unaenda wapi
unafanya nini
lakini wapo kwa
ajili ya kukulinda
wewe.”


“Wanatulinda
sisi kwa ajili
gani?” aliuliza
kwa wasiwasi
Jonathan.





Mama yao
alitabasam
na kuendelea
kuwaelekeza.
“Kila siku,
mnapoenda shule
na mnavyocheza
nje, kuna
wadudu wadogo
wadogo kama
kupe na virusi
wanaokufanya
uumwe. Askari
wako wanasadida
kukulinda. Muda
wote wanafanya
virusi na kupe
wakukimbie
wewe ili
wasikudhuru.”

“Askari wako
wanaposhinda
unajisikia vizuri
na mwenye afya
na nguvu.”





“Lakini kuna
virusi ambavyo
vinaweza
vikashambulia
askari wako,”
alioneza mama
yao. “Ikitokea
kupe na viruksi
vinaweza
vikashambulia
askari wako na
kushinda vita.”

“Usipotumia
dawa vizuri,
askari wako
watashindwa vita
na matokeo yake
utaumwa.”







“Ukinywa
dawa vizuri,
virusi vinakuwa
vimelala kila
wakati na askari
wako wanakuwa
na uwezo
na nguvu za
kukulinda.”

“Lakini mama,
mimi sipendi
kunywa dawa.
Zinanifanya nilale
na kuniumiza
tumbo.”

“Ndio,” alisema
Jonathan “Muda
mwingine
napata upele na
zinanifanya nisikie
kizunguzungu!”





“Wanangu,” alisema mama yao. “Mko sahihi. Muda mwingine vidonge vinaweza vikawafanya mjisikie vibaya, ndio maana tunatakiwa kwenda kumuona daktari kwa ajili ya uchunguzi, ndio maana madaktari wanatubadilishia dawa.”

“Unaweza kumwambia au kumuuliza daktari chochote,” alisema mama yao. “Daktari ni rafiki yako.”

“Lakini mnatakiwa kunywa dawa kila siku kuwasaidia askari wenu,” alisema mama yao. “Siku zingine wazazi/walezi wakisahau kuwapa dawa mnatakiwa muwakumbushe ikitokea wamesahau wawape dawa.”





“Mama,
nimechanganyikiwa.
Rafiki zangu wengi
mbona hawanywi
dawa kama mimi
kila siku, kwani
wako tofauti na
mimi? Au, mimi
hali yangu ni mbaya
tofauti na watoto
wengine ndio maana
natakiwa kunywa
dawa kila siku?”

“Watoto wengine wanakunywa dawa kusaidia askari na wengine hawanywi, lakini watoto wote duniani ni sawa.”




“Kama unakunywa dawa zako vizuri askari wako watafanya kazi zaidi, sio tu kuzuia virusi na kupe, watasaidia kukufanya ufikie malengo uliyojipangia katika maisha yako.”



“Ukiwa shulenii askari
wako watakusaidia
kusoma vizuri na
kukua vizuri.”




“Unapokuwa kwenye mashindano ya mpira wa miguu, askari wako watakuwepo kukusaidia kufunga magori.”




“Unapomaliza
elimu yako ya chuo
kikuu, askari wako
watasherekea pamoja
na wewe.”

“Haijalishi unafanya
nini kwenye
maisha yako, askari
watakusaidia kufikia
malengo na ndoto
zako.”

“Labda siku moja
utakuwa mwana
muziki maarufu. Na
kama ikiwa hivyo,
askari watakuwa
pamoja kufurahi na
wewe.”





“Labda siku moja
utakuwa mwigizaji
maarufu, kama
ikiwa hivyo askari
watakuwepo
unaporekodi filamu
yako.”

“Labda siku moja
utakuwa msanifu
maarufu wa
majengo marefu,
kama ikiwa hivyo
askari watakuwepo
kukusaidia.”





“Labda siku moja
utaoa/utaolewa
na utakuwa na
watoto wako,
kama ikiwa hivyo
askari watakuwepo
kuilinda familia
yako.”



“Askari wako ni ufunguo wa maisha mazuri, na ndio sababu unatakiwa kunywa dawa kila siku.”

“Sasa tumeelewa
kwa nini
tunatakiwa
kunywa dawa,”
alisema Agness na
kuchukua dawa
zake. “Hizi dawa
zinasaidia askari
wangu, na askari
ndio wanoatufanya
tuwe na afya nzuri
na furaha.”



“Usiku mwema,
watoto wangu,”
alisema mama
yao. “Mlale salama
mkijua askari wenu
wapo kuwalinda.”





